# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

## *Cheti cha Ithibati*

Na. 1495

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Shule za Sekondari Kidato cha I - IV

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania

ISBN: 978-9987-743-15-5

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 27 Mei 2024 kuwa Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Shule za Sekondari Kidato cha I - IV nchini Tanzania.

**Dkt Lyabwene M. Mtahabwa**

Kamishna wa Elimu

© Tanzania Islamic Studies Teaching Association (TISTA)

Toleo la 2023

ISBN 978-9987-743-15-5

Tanzania Islamic Studies Teaching Association (TISTA)

S.L.P 55014,
Dar es Salaam - Tanzania, Simu:
+255-784267762, Baruapepe:
tistatz23@gmail.com

Muhtasari huu urejelewe kama: Tanzania Islamic Studies Teaching Association (2023). Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Shule za Sekondari, Kidato cha I – IV.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Tanzania Islamic Studies Teaching Association.

# Yaliyomo


Orodha ya Majedwali.......................................................................... iv

Vifupisho..........................................................................................v

Shukuran..........................................................................................vi

1.0 Utangulizi.......................................................................................1

2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania....................................................1

3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV -Elimu ya Jumla .....2

4.0 Malengo ya Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu Sekondari Kidato cha I–IV................. ......................................... ......................3

5.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV Elimu ya Jumla ............................................................. ......................3

6.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ............... ..................................... ......................4

7.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........................................... ......................5

7.1 Mwalimu.........................................................................................4

7.2 Mwanafunzi ......................................................... .................... 6

7.3 Mzazi/Mlezi......................................................... ......................6

8.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji .............................. ......................6

9.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji.............................. ......................6

10.0 Upimaji............................................................... ......................7

11.0 Idadi ya Vipindi ..................................................... ......................8

12.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji......................... ......................8

Kidato cha I .............................................................. ......................9

Kidato cha II .............................................................. .....................20

Kidato cha III ............................................................. .....................31

Kidato cha IV ............................................................ .....................46

Bibliografia ............................................................... .....................55

# Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Kidato cha I – IV………….……...................................…. 4

Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa Alama za Upimaji Endelevu na Tamati………………..................................... 7

Jedwali Na. 3: Maudhui ya Kidato cha I………………………….…...……... 9

Jedwali Na. 4: Maudhui ya Kidato cha II……………………………....….. 20

Jedwali Na. 5: Maudhui ya Kidato cha III……………………………...….... 31

Jedwali Na. 6: Maudhui ya Kidato cha IV…………………………….......... 46

# Vifupisho

| | | |
|---|---|---|
| A.S | : | Alayhis Salaam (Amani iwe juu yake) |
| IEP | : | Islamic Education Panel |
| LAT | : | Lugha ya Alama ya Tanzania. |
| S.A.W | : | Swalallaahu `Alayhi Wasallam (Rehma na Amani za Allaah ziwe juu yake) |
| S.W | : | Subhaanahu Wata`ala (Mtukufu Aliye juu) |
| TEHAMA | : | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | : | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| TISTA | : | Tanzania Islamic Studies Teaching Association |

## Shukurani

Kila sifa njema anastahiki Allaah (S.W) Mola na Mlezi wa viumbe vyote. Rehma na amani zimuendee Mtume wetu Muhammad (S.A.W), Maswahaba zake pamoja na wafuasi wake wote.

Uandaaji wa Muhtasari wa Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu, Kidato cha I - IV umefanywa na jopo la wataalamu wa Kiislamu. Wataalamu hawa wamefanya kazi kwa weledi mkubwa kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwaandaa wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kuishi kwa uadilifu katika jamii na kuwa raia wema.

Aidha, tunatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kwa utaalamu elekezi pamoja na uwezeshaji wa kazi hii.

Tunamuomba Allaah (S.W) aubariki muhtasari huu ili uweze kutekelezeka na kuleta manufaa kwa watoto wetu. Ee Mola wetu! Tupe rehma itokayo kwako, na ututengenezee uongofu katika kila jambo letu. Aamin!



Dkt. Sheikh Abubakar bin Zubeir bin Ally Mbwana

Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania

Kiongozi Mkuu wa Tanzania Islamic Studies Teaching Association.

## 1.0 Utangulizi

Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni moja ya masomo chaguzi katika Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV kwa wanafunzi wote.

Lengo la kujifunza somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni kumjengea mwanafunzi mwelekeo wa kuielewa Qur'an na Sunnah ya Mtume Muhammad (S.A.W) kama chemchem za mafundisho ya dini ya Kiislamu. Ujifunzaji wa somo hili utakuza maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaomuwezesha mwanafunzi kutambua uwepo wa Allaah (S.W) na sifa zake kisha kumpenda na kumtukuza inavyostahiki, kutekeleza nguzo za Uislamu kwa usahihi na kufuata mwenendo wa Mtume Muhammad (S.A.W) katika maisha ya kila siku. Vilevile, mwanafunzi atakuwa na uwezo wa kumuabudu Allaah (S.W) kwa kuchunga mipaka yake katika kila kipengele cha maisha ya kila siku, kulingania na kusimamisha haki na uadilifu katika jamii pamoja na kuitumikia jamii katika nyanja mbalimbali.

Aidha, muhtasari umeandaliwa ili kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu Sekondari Kidato cha I - IV katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa maelezo yanayowawezesha walimu kuandaa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa ufanisi. Vilevile, muhtasari unatoa nafasi kwa mwalimu kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu zitakazokuza stadi za karne ya 21 zikiwemo ubunifu, mawasiliano, ushirikiano, fikra tunduizi na utatuzi wa changamoto.

Muhtasari huu unachukua nafasi ya muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu shule za sekondari Kidato cha I - IV wa mwaka 2012. Muhtasari wa mwaka 2012 ni matokeo ya maboresho ya muhtasari wa mwaka 2007 uliotokana na maboresho ya muhtasari wa mwaka 1996 ambao ulitokana na maboresho ya muhtasari wa kwanza wa mwaka 1976.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya Elimu nchini Tanzania ni kumuwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Kitanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa, ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV -Elimu ya Jumla

Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV Elimu ya Jumla ni:

(a) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi na mwelekeo alioupata katika hatua ya Elimu ya Msingi;

(b) Kulinda mila na desturi, umoja wa kitaifa, tunu za taifa, demokrasia, kuthamini haki za binadamu na za kiraia, wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo;

(c) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, na kiufundi;

(d) Kuimarisha mawasiliano kwa kutumia stadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha mguso, lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha moja nyingine ya kigeni;

(e) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia na utunzaji endelevu wa mazingira;

(f) Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake, na

(g) Kukuza utayari wa kujiendeleza na mafunzo ya elimu ya kati na ya juu.

## 4.0 Malengo ya Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu Sekondari Kidato cha I–IV

Mwanafunzi anayesoma somo hili, baada ya kumaliza kidato cha nne anatarajiwa amudu:

(a) Kuishi kwa mujibu wa itikadi ya Kiislamu;

(b) Kutekeleza nguzo za Uislamu ipasavyo;

(c) Kutumia sharia na kanuni za Kiislamu katika maisha ya familia na maisha ya jamii;

(d) Kuchambua Qur'an kwa shabaha ya kupata mwongozo wa Allaah (S.W);

(e) Kuchambua Sunnah na Hadithi kwa shabaha ya kumuiga Mtume Muhammad (S.A.W);

(f) Kutumia kanuni zilizopelekea matukio mbalimbali ya historia ya Uislamu kuendeleza na kudumisha haki na uadilifu katika jamii;

(g) Kutumia mafundisho ya Uislamu katika kuamiliana na jamii kwa lengo la kujenga umoja, amani na upendo; na

(h) Kukuza utayari wa kujiendeleza na mafunzo ya elimu ya kati na ya juu.

## 5.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV - Elimu ya Jumla

Umahiri wa jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV - Elimu ya Jumla ni:

(a) Kutumia maarifa na stadi alizozipata katika hatua ya elimu ya sekondari kuimarisha na kupanua uelewa wa kitaaluma;

(b) Kuthamini uraia na Tunu za Taifa;

(c) Kuonesha kujiamini katika kujifunza nyanja mbalimbali zikiwemo Sayansi na Teknolojia, maarifa ya kinadharia na kiufundi;

(d) Kutumia stadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha moja nyingine ya kigeni katika kuwasiliana;

(e) Kutumia maarifa ya masuala mtambuka kuyamudu mazingira yanayomzunguka; na

(f) Kutumia ujuzi na stadi kumwezesha kujiajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha na mazingira.

## 6.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu

Umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu Kidato cha I – IV umebainishwa katika Jedwali Na.1.

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Kidato cha I – IV*

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 1. Kumtambua, kumpenda, kumtukuza na kumsifu Allaah (S.W). | 1.1 Kutambua uwepo wa Allaah (S.W) na sifa zake.<br>1.2 Kuisoma Qur'an kwa mazingatio ya hukumu na ujumbe.<br>1.3 Kuishi kwa kuzingatia Sunnah ya Mtume Muhammad (S.A.W). |
| 2. Kumtumikia Allaah (S.W) katika kila kipengele cha maisha. | 2.1 Kutekeleza nguzo za Uislamu kwa kuzingatia lengo la kila nguzo.<br>2.2 Kuchunga mipaka ya Allaah (S.W) katika kuendesha maisha ya binafsi na jamii. |
| 3. Kulingania na kusimamisha Haki na Uadilifu katika jamii. | 3.1 Kutumia Qur'an na Sunnah kulingania Uislamu katika jamii.<br>3.2 Kutumia historia ya Uislamu kujenga mwenendo mwema wa jamii. |

## 7.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi. Majukumu yao ni kama yafuatayo:

### 7.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

(a) Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu;

(b) Kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai, na uwezo wa mwanafunzi ili kumwezesha:

(i) Kujenga umahiri unaohitajika katika Karne ya 21; na

(ii) Kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

(c) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zile zinazomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali. Mbinu za kufundishia na kujifunzia zinazopendekezwa ni pamoja na; kazi za vitendo, utafiti, majadiliano na kazimradi zinazolenga kutatua matatizo halisi katika mazingira ya mwanafunzi. Aidha, mwalimu anahimizwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa;

(d) Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;

(e) Kutengeneza au kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;

(f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo zikiwemo bunguabongo, orodhahakiki, majaribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi. Zana na mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mtihani wa mwisho;

(g) Kuhakikisha kuwa ufundishaji na ujifunzaji unafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;

(h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;

(i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;

(j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;

(k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa mwanafunzi; na

(l) Kuchopeka masuala mtambuka naTEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 7.2 Mwanafunzi

Mwanafunzi anatarajiwa:

(a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa ili kupata Umahiri unaokusudiwa; na

(c) Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali vikiwemo vitabu vya kiada, ziada na machapisho mengine kutoka katika maktaba mtandao.

### 7.3 Mzazi/Mlezi

Mzazi/Mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;

(b) Kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma pale inapowezekana;

(c) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji;

(d) Kufuatilia mwenendo wa tabia ya mtoto;

(e) Kumpatia mtoto vifaa vyote vinavyohitajika katika ujifunzaji;

(f) Kuhakikisha mtoto anapata mahitaji muhimu; na

(g) Kumfundisha mtoto umuhimu na thamani ya elimu na kazi pamoja na kumhimiza kujifunza kwa bidii.

## 8.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ni msingi katika kujenga umahiri kwa mwanafunzi. Muhtasari huu umependekeza mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila shughuli. Mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji.

## 9.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unahitaji zana mbalimbali ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Hivyo pamoja na zana zinazopendekezwa, mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kushirikiana katika kuandaa au kufaragua zana mbadala zinazopatikana katika mazingira ya shuleni na nyumbani pindi

zinapohitajika. Mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ili kuleta ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

## 10.0 Upimaji

Upimaji ni mchakato muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Mwalimu anashauriwa kuwa na uwanja mpana wa uchaguzi wa mbinu na zana za upimaji ili kupima uwezo wa mwanafunzi wa kusoma Qur'an,kutafsiri Qur'an, kuchambua,kuchanganua na kufafanua kwa usahihi katika miktadha mbalimbali kama vile kuchambua historia ya manabii kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W), kufafanua adabu za matendo ya Muislamu ya kila siku, na kueleza ufahamu wa shahada. Aidha,upimaji utajumuisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na uhitaji wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Zana za upimaji zinazoweza kutumika katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ni orodha hakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, bungua bongo, maswali ya ana kwa ana, kazi kwa vitendo, kazi binafsi na kazi za vikundi, kazimradi na mkoba wa kazi na zana nyingine kama hizo. Hivyo, upimaji endelevu utachangia asilimia 30 ya upimaji wote na upimaji tamati wa kuhitimu Kidato cha Nne utachangia asilimia 70.

Mgawanyo wa alama za upimaji endelevu na tamati umebainishwa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2:** *Mgawanyo wa Alama za Upimaji Endelevu na Tamati*

| Na. | Aina ya upimaji | Asilimia |
|---|---|---|
| 1 | Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha II | 10.0 |
| 2 | Mtihani wa Muhula wa Mwisho wa Kidato cha III | 5.0 |
| 3 | Kazimradi inayofanyika mwishoni mwa Kidato cha III | 5.0 |
| 4 | Mtihani wa Utamilifu wa Kidato cha IV | 10.0 |
| 5 | Mtihani wa kuhitimu Kidato cha IV | 70.0 |
| | **Jumla** | **100.0** |

## 11.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za ujifunzaji. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi viwili (2) kwa wiki sawa na vipindi 70 kwa mwaka wenye wiki 35 za ufundishaji darasani.

## 12.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji yamepangiliwa katika vipengele saba, ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa ,vigezo vya upimaji, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa pamoja na idadi ya vipindi.Maudhui hayo yameoneshwa katika Jedwali Na.3- 6.

## Kidato cha I

**Jedwali Na. 3:** *Maudhui ya Kidato cha I*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0. Kumtambua, kumpenda, kumtukuza na kumsifu Allaah (S.W). | 1.1 Kutambua uwepo wa Allaah (S.W) na sifa zake. | (a) Kufafanua dhana ya Elimu kwa mtazamo wa Uislamu. *(Maana, lengo, chanzo na umuhimu wa elimu, sifa za mtu aliyeelimika, mgawanyo wa Elimu, umuhimu wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu, uhusiano wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu na masomo mengine).* | **Bunguabongo na majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kubungua bongo kisha wajadiliane kwa kufafanua:<br>(i) Maana ya Elimu,<br>(ii) Sifa za mtu aliyeelimika,<br>(iii) Chanzo cha Elimu zote<br>(iv) Umuhimu na lengo la Elimu.<br>(v) Mgawanyo wa Elimu<br>(vi) Umuhimu wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.<br>(vii) Uhusiano wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu na masomo mengine.<br>Baada ya majadiliano, mmoja katika kundi awasilishe darasani. | Dhana ya Elimu imefafanuliwa. | - Kitabu cha kiada kidato cha 1<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya sheikh Abdullah Saleh Farsy<br>- TEHAMA | 2 |
| | | (b) Kuchambua dhana ya dini kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah. *(Maana ya dini, aina za dini)* | **Fikiri – jozisha – shirikisha:** Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kupitia fikiri – jozisha - shirikisha kufafanua<br>(i) Maana ya dini kwa mtazamo wa Qur'an na Sunnah | Kuchambua dhana ya dini kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 1<br>- Tafsiri ya Qur'an ya sheikh Abdullah Saleh Farsy<br>- TEHAMA | 2 |

| mahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | (ii) Aina za dini kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah,<br>Kila kundi kutoa muwakilishi mmoja kuwasilisha walichojifunza. | | | |
| | | (c) Kuchambua dhana ya Imani kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah.<br>*(Maana, nguzo za Imani na nguzo ya ihsani, sifa za muumini wa kweli katika aya za Quran; (49:15), ( 8:2 – 4), (2:2 – 5), (23:1-11)* | **Bunguabongo na majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi kubungua bongo kisha wajadiliane juu ya<br>(i) Maana ya Imani<br>(ii) Nguzo za Imani na nguzo ya Ihsan<br>(iii) Sifa za muumini wa kweli kwa mujibu wa Quran; (49:15), (8:2 – 4), (2:2 – 5), (23:1-11) | Kuchambua dhana ya Imani kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 1<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy<br>- TEHAMA<br>- Matini mbalimbali kuhusu Imani ya Kiislamu. | 4 |
| | | (d) Kufafanua dhana ya Tawhiid na shirki.<br>*(Maana,namna ya kumpwekesha Allaah (SW), umuhimu wa Tawhiid, aina za shirki, madhara ya shirki)* | **Bunguabongo:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi kubungua bongo juu ya maana ya Tawhiid<br>**Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi kujadiliana juu ya umuhimu wa Tawhiid, aina na madhara ya shirki. | Dhana ya Tawhiid na shirki imefafanuliwa. | - Kitabu cha kiada kidato cha I<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy<br>- TEHAMA<br>- Matini mbalimbali kuhusu Tawhiid. | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kuisoma Qur'an kwa mazingatio ya hukumu na ujumbe. | (a) Kuchambua dhana ya Qur'an. *(Maana, kushuka, namna ilivyo hifadhiwa na misingi ya kuifahamu)* | **Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo wajadiliane kisha kuwasilisha kwa zamu mbele ya wenzao darasani walichojifunza juu ya<br>(i) Maana ya Qur'an<br>(ii) Historia ya kushuka kwa Qur'an<br>(iii) Njia zilizotumika kuhifadhi Qur'an<br>(iv) Misingi ya kuifahamu Qur'an. | Kuchambua dhana ya Qur'an kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha I<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya sheikh Abdullah Saleh Farsy<br>- TEHAMA | 2 |
| | | (b) Kuchambua dhana ya usomaji wa Qur'an. *(umuhimu wa kusoma Qur'an kwa kuzingatia hukumu za Tajwiid, hukumu za nun sakina na tanwin)* | **Majadiliano**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kujadiliana kisha kuwasilisha walichojifunza juu ya:<br>(i) umuhimu wa kusoma Qur'an kwa kuzingatia hukumu za Tajwiid.<br>(ii) hukumu za nun sakina na tanwin, | Kuchambua dhana ya usomaji wa Qur'an kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 1<br>- Matini mbalimbali kuhusu Tajwiid.<br>- Juzuu Amma | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuchambua sura zilizoteuliwa: Al-Fat-ha (1); An-Naas (114); Al-Falaq (113); Ikhlas (112).<br><br>*(Kusoma kwa hukumu, kuhifadhi, kutafsiri na kueleza mafunzo ya kila sura)* | **Kazimradi;**<br>Waongoze wanafunzi katika vikundi wakutane kwa muda wao wa ziada nje ya darasa kusoma kwa hukumu, kuhifadhi, kutafsiri sura zifuatazo:<br>Al – Fat-ha (1), An Naas (114), Falaq (113) na Ikhlas (112) wang'amue mafunzo katika kila sura, kisha kuwasilisha kazi zao baada ya muda waliopewa kukamilika.<br>**Majadiliano;**<br>Jadiliana na wanafunzi namna ya kutekeleza ujumbe wa sura walizojifunza. | Kuchambua sura zilizoteuliwa kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 1<br>- TEHAMA<br>- Tafsiri ya Qur'an ya sheikh Abdullah Saleh Farsy | 6 |
| | 1.3 Kuishi kwa kuzingatia Sunnah ya Mtume Muhammad (SAW) | (a) Kuchambua dhana ya Sunnah na Hadithi.<br>*(Maana, umuhimu na tofauti ya Sunnah na Hadithi, kazi ya Sunnah)* | **Fikiri – jozisha – shirikishi:**<br>Waongoze wanafunzi kupitia fikiri – jozisha – shirikishi kufafanua maana na umuhimu wa Sunnah na Hadithi.<br>**Majadiliano:**<br>Waongoze wanafunzi kupitia majadiliano katika vikundi kueleza tofauti ya Sunnah na Hadithi na kazi ya sunnah. | Kuchambua dhana ya Sunnah na Hadithi kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 1<br>- Matini ya Hadithi zilizoteuliwa<br>- Tafsiri ya Riyadhus Salihin. | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuchambua Hadithi zilizoteuliwa kuhusu Ikhlas, kujiheshimu na kuheshimu wazazi, viongozi na wakubwa, kuwa mpole na mnyenyekevu, kuwa mkweli na kujiepusha na uongo, kuwa mwaminifu na mwadilifu, kuchunga ahadi, kujiepusha na maongezi ya kipuuzi, kuwa na upendo, adabu za kunyoa/ kusuka nywele<br>*(Kusoma kwa kuhifadhi, kuandika, kutafsiri na kubainisha mafunzo)* | **Kazimradi;**<br>Waongoze wanafunzi katika vikundi wakutane kwa muda wao nje ya darasa kusoma kwa kuhifadhi, kuandika na kutoa tafsiri pamoja na kutoa mafunzo ya Hadithi kuhusu Ikhlas, kujiheshimu na kuheshimu wazazi, wakubwa na viongozi, kuwa mpole na mnyenyekevu, kuwa mkweli na kujiepusha na uongo, kuwa mwaminifu na mwadilifu, kuchunga ahadi, kujiepusha na maongezi ya kipuuzi, kuwa na upendo, adabu za kunyoa/kusuka nywele<br>**Matembezi ya galari;**<br>Ongoza wanafunzi kuorodhesha mafunzo yatokanayo na Hadithi husika na kubandika kwenye kuta za darasa, kufanya matembezi na kuulizana maswali katika vikundi mbalimbali.<br>**Fikiri - andika - jozisha - shirikisha;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kutafakari na kuandika mapendekezo namna ya kutekeleza mafunzo ya Hadithi husika kisha ufanye majumuisho. | Kuchambua Hadithi zilizoteuliwa kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 1<br>- Tafsiri ya Riyadhus Salihin. | 6 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kumtumikia Allaah (S.W) katika kila kipengele cha maisha | 2.1 Kutekeleza nguzo za Uislamu kwa kuzingatia lengo la kila nguzo. | (a) Kufafanua dhana juu ya Uislamu na nguzo za Uislamu kwa mujibu wa Qur an na Sunnah *(Maana, sifa za Muislamu, lengo, umuhimu wa kila nguzo)* | **Maswali na majibu;** Ongoza wanafunzi Kusoma matini uliyoandaa kisha kujibu maswali uliyoandaa ili kubaini<br>(i) Maana ya Uislamu.<br>(ii) Sifa za Muislamu<br>(iii) Maana ya kila nguzo ya Uislamu<br>(iv) Lengo la kila nguzo ya Uislamu<br>(iv) Umuhimu wa nguzo za Uislamu.<br>(v) Tofauti kati ya Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano na Uislamu ni nguzo tano | Dhana juu ya nguzo za Uislamu imefafanuliwa. | - Kitabu cha kiada kidato cha I<br>- Mchoro wa Jengo<br>- Tafsiri ya Qur'an ya sheikh Abdullah Saleh Farsy<br>- TEHAMA | 4 |
| | | (b) Kueleza dhana ya Shahada. *(Kutamka shahada mbili kwa matini ya kiarabu, Tafsiri ya shahada, hatua za shahada, umuhimu wa shahada)* | **Fikiri – jozisha – shirikisha:** Ongoza wanafunzi kupitia fikiri – jozisha – shirikisha kusoma matini uliyoandaa ili waweze:<br>(i) kutamka shahada mbili<br>(ii) kutafsiri shahada mbili<br>(iii) kubainisha hatua tatu za shahada<br>(iv) kueleza umuhimu wa shahada | Kueleza dhana ya shahada kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 1 Chati/jedwali,<br>- ya Qur'an ya sheikh Abdullah Saleh Farsy<br>- TEHAMA | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kufafanua utekelezaji wa swala za faradhi: *(twahara- udhu, josho, tayamamu, kuondoa najisi), kuelekea qibla, kujisitiri, kuingia kwa wakati) nguzo, Sunnah, Makruh na yanayobatilisha sala, namna ya kuswali swala za jamaa na swala ya ijumaa , kuswali nyakati za dharura safarini, mgonjwa na vitani,)* | **Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kupitia majadiliano katika vikundi kufafanua<br>(i) nguzo na Sunnah za swala<br>(ii) namna ya kuswali nyakati za dharura - safarini, mgonjwa na vitani,<br>(iii) namna ya kuswali swala za jamaa.<br>**Oneshombinu:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi kuswali kwa kuzingatia masharti, nguzo na Sunnah, Makruh na yanayobatilisha swala, namna ya kuswali swala za jamaa na swala ya ijumaa , kuswali nyakati za dharura safarini, mgonjwa na vitani). | Utekelezaji wa swala za faradhi umefafanuliwa. | - Kitabu cha kiada kidato cha 1<br>- Dira, maji safi, vifaa vya kutilia udhu<br>- Michoro mbalimbali<br>- Mswala<br>- Tafsiri ya Qur'an ya sheikh Abdullah Saleh Farsy<br>- TEHAMA<br>- Manila kadi | 6 |
| | | (d) Kubainisha swala za sunnah *(Swala za Iddi, Tarawehe, witri, Qabliyyah na Ba'adiyyah, Dhuha, Tahiyyaatul masjid, Qiyaamullayl na Istikhara).* | **Fikiri – jozisha – shirikisha:**<br>Ongoza wanafunzi kupitia fikiri – jozisha – shirikisha kusoma matini uliyoandaa ili waweze kubainisha:<br>Swala za Iddi, Tarawehe, swala ya witri, Qabliyyah na Ba'adiyyah, Dhuha, tahiyyaatul – masjid, Qiyaamullayl na Istikhara. | Kubainisha swala za sunnah kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha I.<br>- TEHAMA | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kufafanua mambo anayostahiki kufanyiwa maiti wa Kiislamu. *(Kuoshwa, kuvishwa sanda, kuswaliwa na kuzikwa).* | **Igizodhima:** Ongoza wanafunzi kufanya igizo ili kuchanganua mambo anayofanyiwa maiti wa Kiislamu<br>(i) Hatua za kumuosha, kumvika sanda na kumswalia<br>(ii) sharti na nguzo za swala ya maiti<br>(iii) namna ya kumswalia maiti<br>(iv) kuandaa kaburi na namna ya kumzika maiti. | Mambo anayostahiki kufanyiwa maiti muislamu yamefafanuliwa. | - Kitabu cha kiada kidato cha 1<br>- Vitu halisi – sanda, maji n.k)<br>- Mahali pa kuoshea maiti<br>- TEHAMA | 4 |
| | 2.2 Kuchunga mipaka ya Allaah (S.W) katika kuendesha maisha ya binafsi na jamii | (a) Kuchambua dhana ya Fiqh. *(maana ya Fiqh, matapo ya Fiqh, chimbuko, na umuhimu wa fiqh)* | **Fikiri – jozisha – fikirisha:** Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kupitia fikiri – jozisha – fikirisha kufafanua:<br>(i) Maana ya Fiqh<br>(ii) Matapo ya Fiqh<br>(iii) Chimbuko la fiqh<br>(iv) Umuhimu wa Fiqh<br>Kisha mmoja wao katika kikundi kuwasilisha | Kuchambua dhana ya fiqh kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha I<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy<br>- TEHAMA | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kufafanua misingi na vyanzo vya sharia za Kiislamu *(Qur an, Sunnah na Ijtihad).* | **Fikiri – jozisha – fikirisha:** Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kupitia fikiri – jozisha – fikirisha kufafanua misingi na vyanzo vya sharia za Kiislamu. kisha mmoja wao katika kikundi kuwasilisha walichojifunza | Kufafanua misingi na vyanzo vya sharia za Kiislamu kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha I<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy<br>- TEHAMA | 2 |
| 3.0 Kulingania na kusimamisha haki na uadilifu katika jamii | 3.1 Kutumia Qur'an na Sunnah kulingania uislamu katika jamii. | (a) Kuchambua dhana ya kulingania Uislamu katika jamii (da`awah). *(Maana, lengo, misingi, umuhimu na faida).* | **Fikiri – jozisha – fikirisha:** Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kuchambua<br>(i) maana, misingi na lengo la kulingania<br>(ii) Umuhimu wa kulingania Uislamu na faida zake.<br>Kisha mmoja wao katika kikundi kuwasilisha walichojifunza na ufanye majumuisho. | Kuchambua dhana ya kulingania Uislamu katika jamii kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha I<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy. | 4 |
| | | (b) Kufafanua nguzo za da`awah *(Da`i, hadhira na ujumbe).* | **Majadiliano na Maswali na majibu:** Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kupitia majadiliano kufafanua nguzo tatu za da`awah ambazo ni da`i, hadhira na ujumbe. Kisha ufanye majumuisho. | Kufafanua nguzo za da`awah kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha I<br>- Bango kitita<br>- Matini mbalimbali kuhusu nguzo za da`awah. | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kutumia historia ya Uislamu kujenga mwenendo mwema wa jamii. | (a) Kufafanua dhana ya historia ya mwanadamu kwa mujibu wa Uislamu. *(Tofauti ya mtazamo wa Uislamu na ule wa makafiri juu ya maana, umuhimu wa historia,lengo la kuumbwa mwanadamu na hadhi yake hapa ulimwenguni).* | **Bunguabongo:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kufafanua maana ya historia kwa mtazamo wa Uislamu.<br>**Majadiliano na Maswali na majibu:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kupitia majadiliano kufafanua;<br>(i) Umuhimu wa historia<br>(ii) Tofauti ya mtazamo wa Uislamu na ule wa makafiri juu ya historia<br>(iii) Mtazamo wa Uislamu juu ya lengo la kuumbwa mwanadamu na hadhi yake<br>Kila kikundi kitoe muwakilishi mmoja awasilishe walichojifuza. | Dhana ya historia ya mwanadamu kwa mujibu wa Uislamu imefafanuliwa. | - Kitabu cha kiada kidato cha I<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy<br>- TEHAMA<br>- Matini mbalimbali kuhusu historia ya mwanadamu kwa mujibu wa Uislamu. | 2 |
| | | (b) Kuchambua historia ya nabii Adam (A.S), *(Kuumbwa, maisha ya peponi, kuteremshwa ardhini na maisha ya watoto wake).* | **Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi kujadiliana katika vikundi mafunzo yatokanayo na historia ya nabii Adam (A.S). | Kuchambua Historia ya nabii Adam (A.S) kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha I<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy<br>- Matini mbalimbali kuhusu Historia ya nabii Adam (A.S). | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuchambua historia ya manabii kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W): Nuhu (A.S), Ibrahim (A.S), Lut (A.S), Musa (A.S); na Isa (A.S). *(wasifu, hali ya jamii zao, mbinu za kulingania na mafunzo yatokanayo katika kujenga jamii bora).* | **Majadiliano:** Ongoza wanafunzi kujadiliana katika vikundi mafunzo yatokanayo na historia ya manabii (Nuhu (A.S), Ibrahim (A.S), Lut (A.S), Musa (A.S); na Isa (A.S))<br>**Matembezi ya galari:** Ongoza wanafunzi kufanya matembezi ya galari baada ya majadiliano ili kujifunza mafunzo yatokanayo na historia ya manabii. | Kuchambua Historia ya Manabii kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W) kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha I<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy<br>- TEHAMA<br>- Matini mbalimbali kuhusu Historia ya Manabii kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W). | 6 |

## Kidato cha II

**Jedwali Na. 4:** *Maudhui ya Kidato cha II*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumtambua, kumpenda, kumtukuza na kumsifu Allaah (S.W). | 1.1 Kutambua uwepo wa Allaah (S.W) na sifa zake. | (a) Kufafanua dhana ya dini kwa mujibu wa Qur'an. *(tofauti ya mtazamo wa Uislamu na ukafiri juu ya chanzo na kazi ya dini, sababu za hitajio la dini kwa mwanadamu).* | **Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kusoma matini uliyoandaa waweze kujifunza kisha kufafanua.<br>(i) tofauti kati ya mtazamo wa Uislamu na mtazamo wa kikafiri juu ya chanzo na kazi ya dini katika jamii,<br>(ii) sababu za hitajio la dini kwa mwanadamu.<br>Kila kikundi kuwepo mwakilishi wa kuwasilisha walichojifunza mbele ya darasa. | Kufafanua dhana ya dini kwa mujibu wa Qur'an kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>- Matini mbalimbali kuhusu ufahamu wa dini kwa mujibu wa Qur'an<br>- Bango kitita | 4 |
| | | (b) Kufafanua njia za kumjua Allaah (S.W) na kuthibitisha kuwepo kwake *(njia za kumjua Allaah, kumuamini Allah sio sualla la kibubusa, udhaifu wa madia ya makafiri dhidi ya kuwepo Allaah (S.W), dalili za kuwepo Allaah (S.W), Athari za kumuamini Allaah (S.W) katika maisha ya kila siku.* | **Utafiti mdogo:** elekeza wanafunzi kusoma matini ulioandaa ya njia za kumjua Allaah (S.W) na kuandika maelezo yao binafsi kuhusu nafasi ya fitra na akili katika kumtambua Allaah (S.W).<br>**Majadiliano;** Ongoza wanafunzi katika vikundi kusoma matini uliyoandaa kisha kujadiliana juu ya kuonesha kuwa, kumuamini Allaah (S.W) si suala la kufuata mkumbo: | Kufafanua njia za kumjua Allaah (S.W) na kuthibitisha kuwepo kwake kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdulla Saleh Farsy<br>- TEHAMA.<br>- Matini mbalimbali<br>- TEHAMA | 6 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | (ii) Udhaifu wa madai ya makafiri dhidi ya kuwepo kwa Allaah (S.W)<br>(iii) dalili za kuthibitisha kuwepo kwa Allaah (S.W). (mbingu, ardhi na vilivyomo, umbile la mwanadamu, historia ya mwanadamu, maisha ya mitume na mafundisho ya mitume)<br>(iv) Athari za kumuamini Allaah (S.W) katika maisha ya kila siku. | | | |
| | | (c) Kuchambua sifa na majina 99 ya Allaah (S.W) *(kuyasoma, kuyahifadhi na kuyazingatia).* | **Kazi mradi**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kujadiliana kisha kuwasilisha walichojifunza juu ya:<br>(i) Sifa na majina ya Allaah (SW).<br>(ii) Baada ya muda waliopewa kukamilika, waongoze wanafunzi wakutane kwa muda wao nje ya darasa kusoma majina ya Allaah (S.W) na tafsiri zake kisha kuwasilisha kazi zao. | Kuchambua sifa na majina ya Allaah (SW) kumefanyika | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>- TEHAMA<br>- Matini mbalimbali kuhusu sifa na majina ya Allaah (SW) | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kuisoma Qur'an kwa mazingatio ya hukumu na ujumbe. | (a) Kuchambua dhana ya hukumu za usomaji wa Qur'an. *(hukumu za mim na nuni zenye shadda, hukumu za mim sakina* | **Majadiliano**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kujadiliana kisha kuwasilisha walichojifunza juu ya:<br>(i) hukumu za mim na nuni zenye shadda,<br>(ii) hukumu za mim sakini | Kuchambua dhana ya usomaji wa Qur'an kumefanyikai. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>- Matini mbalimbali kuhusu tajwiid. | 4 |
| | | (b) Kuchambua historia ya kushuka Qur'an. *(Hatua za kushuka Qur'an, hekima ya Qur'an kushuka hatua kwa hatua, namna Qur'an ilivyohifadhiwa kuanzia wakati ikishuka hadi leo).* | **Bunguabongo:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi kwa maswali ya kufikirisha katika vikundi vidogo vidogo kubungua bongo juu ya<br>(i) Hatua mbili kuu za kushuka Qur'an<br>(ii) Hekima ya Qur'an kushuka hatua kwa hatua<br>(iii) Namna Qur'an ilivyohifadhiwa kuanzia wakati ikishuka hadi leo. | Kuchambua historia ya kushuka Qur'an kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdulla Saleh Farsy<br>- TEHAMA | 2 |
| | | (c) Kuchambua sura zilizoteuliwa: Lahab (111); Nasr (110); Kaafiruun (109); Maa'uun (107). | **Kazimradi;**<br>Waongoze wanafunzi katika vikundi wakutane kwa muda wao wa ziada nje ya darasa kusoma kwa kuhifadhi na kutoa tafsiri ya sura zilizoteuliwa: | Sura zilizoteuliwa zimechambuliwa. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdulla Saleh Farsy<br>- TEHAMA | 8 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *(Kusoma kwa hukumu, kuhifadhi, kutafsiri na kutoa mafunzo).* | Lahab (111), Nasr (110), Kaafiruun (109), na Maa'uun (107)<br>Wabaini mafunzo katika kila sura kisha kuwasilisha kazi zao baada ya muda uliowapa kukamilika.<br>**Majadiliano**<br>Jadiliana na wanafunzi namna ya kutekeleza mafunzo ya sura walizohifadhi. | | | |
| | 1.3 Kuishi kwa kuzingatia Sunnah ya Mtume Muhammad (S.A.W) | (a) Kuchambua historia ya uandishi wa Hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W). *(Wakati wa uhai wa Mtume Muhammad (SAW), Maswahaba, Tabiina, Tabii Taabiina).* | **Maswali na majibu na Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kusoma matini iliyoandaliwa waweze kujifunza na kufafanua historia ya uandishi wa Hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W)<br>(i) Wakati wa uhai wa Mtume Muhammad (S.A.W)<br>(ii) Maswahaba<br>(iii) Taabiin<br>(iv) Taabii taabiina | Kuchambua historia ya uandishi wa Hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W) kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>- Matini mbalimbali kuhusu historia ya uandishi wa Hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W) | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kufafanua Hadithi zilizoteuliwa kuhusu; kuepuka usengenyaji, kujiepusha na dharau, kujiepusha na matusi, kuepuka mabishano, kuepuka kujisifu na kujitukuza, kuepukana na kibri na majivuno, kuepukana na kulaani ovyo, kujiepusha na viapo. *(Kusoma kwa kuhifadhi, kuandika, kutafsiri na kubaini mafunzo).* | **Kazimradi;** Waongoze wanafunzi katika vikundi wakutane kwa muda wao nje ya darasa kusoma kwa kuhifadhi, kuandika na kutoa tafsiri na mafunzo ya Hadithi kuhusu kuepuka usengenyaji, kujiepusha na dharau, kujiepusha na matusi, kuepuka mabishano, kuepuka kujisifu na kujitukuza, kuepukana na kibri na majivuno, kuepukana na kulaani ovyo, kujiepusha na viapo, kujiheshimu na kuheshimu wengine na kuwa mpole na mnyenyekevu kisha kuwasilisha kazi zao baada ya muda waliopewa kukamilika.<br><br>**Matembezi ya galari;** Ongoza wanafunzi kuorodhesha mafunzo yatokanayo na Hadithi husika na kubandika kwenye kuta za darasa, kufanya matembezi na kuulizana maswali katika vikundi mbalimbali. | Kuchambua Hadithi zilizoteuliwa kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>- Tafsiri ya Riyadhus Salihina. | 6 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Fikiri - andika - jozisha - shirikisha;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogovidogo kutafakari na kuandika mapendekezo namna ya kutekeleza mafunzo ya Hadithi husika kisha ufanye majumuisho | | | |
| 2.0 Kumtumikia Allaah (S.W) katika kila kipengele cha maisha. | 2.1 Kutekeleza nguzo za Uislamu kwa kuzingatia lengo la kila nguzo. | (a) Kufafanua utekelezaji wa ibada ya Zakat. *(Masharti, mali zinazopasa kutolewa Zakat, nisaabu na makundi ya watu wanaostahiki kupewa Zakat).* | **Bunguabongo:**<br>Ongoza wanafunzi kuchangia fikra zao ili waweze kueleza maana ya Zakat na Swadaqat na umuhimu wake.<br>**Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi kujadiliana katika vikundi vidogo vidogo juu ya<br>(i) Masharti ya utoaji Zakat na Swadaqat<br>(ii) Nisaab na kiasi cha mali kinachopaswa kutolewa.<br>(iii) Wanaostahiki kupewa Zakat. | Kufafanua utekelezaji wa ibada ya Zakat kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>Bango kitita<br>Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdulla Saleh Farsy<br>TEHAMA<br>Matini mbalimbali kuhusu Zakat na Swadaqat. | 4 |


25

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kufafanua utekelezaji wa ibada ya funga *(Maana, aina, umuhimu, nguzo za funga, sunnah na miiko ya funga, kubatilika kwa funga,)* | **Fikiri – jozisha – shirikisha:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kupitia Fikiri, jozisha, shirikisha<br>Kufafanua<br>(i) Maana.<br>(ii) Aina<br>(iii) Umuhimu<br>(iv) Nguzo, sunnah na miiko ya funga<br>(v) mambo yanayoharibu na kubatilisha funga<br>**Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili masharti, nguzo na Sunnah za funga | Kufafanua utekelezaji wa ibada ya funga kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdulla Saleh Farsy<br>- Matini mbalimbali kuhusu funga. | 4 |
| | 2.2 Kuchunga mipaka ya Allaah (S.W) katika kuendesha maisha ya binafsi na jamii | (a) Kuchambua dhana ya familia ya Kiislamu. *(Maana, umuhimu, na taratibu za ndoa katika Uislamu, umri wa kuoa na kuolewa, majukumu katika familia na ukewenza)* | **Majadiliano na Kuwasilisha;**<br>Wanafunzi wakiwa katika vikundi vidogo vidogo waongoze kueleza<br>(i) Maana ya ndoa ya Kiislamu<br>(ii) Taratibu za kukamilisha ndoa ya Kiislamu<br>(iii) Umri wa kuoa na kuolewa<br>(iv) Majukumu ya mume kwa mke, mke kwa mume, | Kuchambua dhana ya familia ya Kiislamu kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>- Matini mbalimbali kuhusu familia ya Kiislamu<br>- Bango kitita | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | wazazi kwa watoto na watoto kwa wazazi katika familia ya Kiislamu.<br>(v) Ruhusa kwa mume kuoa mke zaidi ya mmoja. | | | |
| | | (b) Kufafanua vipengele vya utamaduni wa Kiislamu *(maana, mavazi, sherehe, misiba, maamkizi, michezo)* | **Changanyakete;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogovidogo kusoma matini kwa kujadiliana kisha kuandaa nukuu zifuatazo<br>(i) Maana ya utamaduni wa Kiislamu<br>(ii) orodha ya vipengele vya utamaduni wa Kiislamu.<br>Elekeza kila kikundi kutoa mwakilishi mmoja kwenda kikundi kingine kufundisha walichojifunza katika kundi lao. | Kufafanua vipengele vya utamaduni wa Kiislamu kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>- Bango kitita | 4 |
| | | (c) Kufafanua adabu za matendo ya Muislamu ya kila siku: *(kula, kwenda haja, kulala na kuamka, kuoga, kutoka na kurudi nyumbani, kupiga miayo na* | **Majadiliano;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kujadiliana adabu za matendo ya Muislamu kwa siku. | Kufafanua adabu za matendo ya Muislamu ya kila siku kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>- Bango kitita | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *chafya, kuishi na watu kwa wema, kuwatembelea wagonjwa, kuingia na kutoka msikitini)* | | | | |
| 3.0 Kulingania na kusimamisha haki na uadilifu katika jamii. | 3.1 Kutumia Qur'an na Sunnah kulingania uislamu katika jamii. | (a) Kufafanua sifa za mlinganiaji. *(Ujuzi sahihi,Imani thabiti, tabia njema, kuendeleza Uislamu kuwe ndio lengo kuu la maisha, kutaraji malipo kutoka kwa Allaah (S.W), kuwa na subira, kuwa na hekima).* | **Majadiliano;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kufafanua na kuandika taarifa kuhusu sifa za mlinganiaji.<br>Kisha wachague muwakilishi wa kila kikundi awasilishe kazi yao mbele ya wenzao na ufanye majumuisho. | Sifa za mlinganiaji zimefafanuliwa. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>- Bango kitita | 2 |
| | | (b) Kuchambua sifa za kundi la walinganiaji. *(Mshikamano wa udugu na upendo, kushauriana, nidhamu na utii, kukosoana kwa nia njema na njia nzuri, kujiepusha na kujiona na ria, kuwa na subira, kuwa na hekima* | **Majadiliano;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kujadiliana na kuandika taarifa kuhusu sifa za walinganiaji.<br>Kisha wachague muwakilishi wa kila kikundi awasilishe kazi yao mbele ya wenzao na ufanye majumuisho. | Kuchambua sifa za walinganiaji kumefanyika | - Kitabu cha kiada<br>- kidato cha 2<br>- Bango Kitita | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kutumia historia ya Uislamu kujenga mwenendo mwema wa jamii | (a) Kufafanua hali ya jamii ya Bara Arabu zama za jahiliya (509 – 609A.D). *(Utabiri wa ujio wa Mtume Muhammad (S.A.W), mifumo ya jamii kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kimaadili, utukufu wa mji wa Makkah na kabila la Quraysh,).* | **Majadiliano**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kusoma matini mbalimbali ili kubainisha utabiri wa ujio wa Mtume Muhammad (S.A.W), mifumo ya jamii kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kimaadili katika bara Arab, utukufu wa mji wa Makkah na kabila la Quraysh, wahusianishe na yanayotokea katika mazingira yao. | Kufafanua hali ya jamii ya Bara Arabu zama za jahiliya (509 – 609A.D) kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdulla Saleh Farsy<br>TEHAMA<br>Matini mbalimbali kuhusu zama za Jahiliya karne ya sita katika bara Arab. | 4 |
| | | (b) Kufafanua mbinu za ulinganiaji alizozitumia Mtume Muhammad (S.A.W) kipindi cha Makkah. *(Kuzaliwa kwa Mtume (S.A.W), kulelewa, nasaba, makuzi, kuandaliwa, kupewa Utume, kulingania, upinzani* | **Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi kusoma matini uliyoandaa waweze kujifunza na kutoa ufafanuzi wa kina juu ya:<br>(i) Kuzaliwa kwa Mtume (S.A.W),<br>(ii) Nasaba na malezi ya Mtume Muhammad (S.A.W),<br>(iii) Maandalizi ya Mtume Muhammad (S.A.W) kabla na baada ya kupewa utume na mafunzo yatokanayo | Kufafanua mbinu za ulinganiaji alizozitumia Mtume Muhammad (SAW) kipindi cha Makkah kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 2<br>Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdulla Saleh Farsy<br>TEHAMA<br>Matini mbalimbali kuhusu Historia ya Uislamu kipindi cha Mtume Muhammad (S.A.W) akiwa Makkah. | 6 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *wa makureishi, isra na miraji, hijra na mafunzo yatokanayo katika kujenga jamii)* | (iv) sababu za makafiri wa Makkah kuupinga Uislamu na mafunzo yatokanayo<br>(v) Mbinu za makafiri katika kuupinga Uislamu Makkah na mafunzo yatokanayo<br>(vi) Jinsi Mtume Muhammad (SAW) alivyoandaa ummah wa waislamu Makkah na mafunzo yatokanayo<br>(vii) Israa na Miraji na mafunzo yatokanayo<br>(viii) Mchakato wa Hijra ya Mtume Muhammad (SAW) na Maswahaba kuhamia Madinah na mafunzo yatokanayo. | | | |

# Kidato cha III

**Jedwali Na. 5:** *Maudhui ya Kidato cha III*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumtambua, kumpenda, kumtukuza na kumsifu Allaah (S.W) | 1.1 Kutambua uwepo wa Allaah (S.W) na sifa zake | (a) Kuchambua nguzo ya kuamini malaika wa Allaah (S.W) *(maana, umuhimu, sifa, kazi na athari ya kuamini malaika katika maisha ya kila siku)* | **Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kusoma matini uliyoandaa ili wajifunze kwa kujadiliana kuhusu<br>(i) Maana ya kuamini Malaika<br>(ii) Umuhimu wa kuamini ya Malaika<br>(iii) Sifa na kazi za Malaika<br>(iv) Athari ya kuamini Malaika katika maisha ya kila siku.<br>Kila kikundi kutoa mwakilishi mmoja kuwasilisha walichojifunza kwa wenzao darasani | Kuchambua nguzo ya kuamini malaika wa Allaah (S.W) kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdulla Saleh Farsy<br>- TEHAMA<br>- Matini mbalimbali kuhusu kuamini malaika wa Allaah (S.W) . | 2 |
| | | (b) Kuchambua nguzo ya kuamini vitabu vya Allaah (S.W). *(Umuhimu wa kuamini vitabu vya Allaah (S.W), lengo la vitabu vya Allaah (S.W), tofauti ya Qur'an na vitabu vingine vya Allaah (S.W),* | **Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi kusoma matini uliyoandaa ili wajifunze kwa kujadiliana juu ya:<br>(i) Umuhimu wa kuamini vitabu vya Allaah (S.W)<br>(ii) Lengo la vitabu vya Allaah (S.W),<br>(iii) Tofauti ya Qur'an na vitabu vingine vya Allaah (S.W) | Kuchambua nguzo ya kuamini vitabu vya Allaah (S.W) kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdulla Saleh Farsy<br>- TEHAMA<br>- Matini mbalimbali kuhusu kuamini vitabu vya Allaah (S.W) | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *Qur an haipitwi na wakati, athari ya kuamini vitabu vya Allaah (S.W) katika maisha ya jamii)* | (iv) Qur'an haipitwi na wakati.<br>(v) Athari ya kuamini vitabu vya Allaah (S.W) katika maisha ya jamii.<br>Kila kikundi kutoa mwakilishi mmoja kuwasilisha mbele ya darasa. | | | |
| | | (c ) Kuchambua dhana ya kuamini mitume wa Allaah (S.W).<br>*(uwepo wa mitume, sifa zao, mafundisho yao mwisho wa utume na taathira ya kuamini mitume katika maisha ya kila siku).* | **Majadiliano na Kuwasilisha;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kubainisha<br>(i) Ushahidi wa uwepo wa mitume<br>(ii) Sifa za mitume<br>(iii) mafundisho ya mitume<br>(iv) Mwisho wa utume<br>(v) Taathira ya kuamini mitume katika maisha ya kila siku. | Kuchambua dhana juu ya kuamini mitume wa Allaah (S.W) kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Matini mbalimbali kuhusu kuamini mitume wa Allaah (S.W).<br>- Bango kitita | 2 |
| | | (d) Kuchambua dhana ya kuamini siku ya mwisho.<br>*(Mazingira ya siku ya mwisho, udhaifu wa madai* | **Majadiliano na Kuwasilisha;**<br>Wanafunzi wakiwa katika vikundi vidogo vidogo waongoze;<br>(i) Kubaini mazingira ya siku ya mwisho | Dhana ya kuamini siku ya mwisho imechambuliwa. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Matini mbalimbali kuhusu Kuamini siku ya mwisho<br>- Bango kitita | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *ya makafiri dhidi ya siku ya mwisho, hoja za kuthibitisha kuwepo kwa siku ya mwisho, ufahamu wa shufaa, athari ya kuamini siku ya mwisho katika maisha ya kila siku)* | (ii) kueleza hoja za makafiri dhidi ya uwepo wa siku ya mwisho na udhaifu wake<br>(iii) Kufafanua hoja za kimantiki na kihistoria kuthibitisha uwepo wa siku ya mwisho<br>(iv) Kueleza shufaa itakavyokuwa siku ya kiyama.<br>(v) Kubaini taathira ya kuamini siku ya mwisho katika maisha ya kila siku. | | | |
| | | (e) Kufafanua dhana ya kuamini Qadar ya Allaah (S.W). *(Maana, tofauti ya Qadar na Qudra, umuhimu, na athari ya kuamini Qadar katika maisha ya kila siku).* | **Fikiri -andika - jozisha -shirikisha:**<br>Ongoza wanafunzi kufikiri, kuandika, kujozisha na kushirikishana katika vikundi kufafanua<br>(i) Maana na tofauti kati ya Qadar na Qudra ya Allaah (S.W)<br>(ii) Umuhimu wa kuamini Qadar ya Allah (S.W)<br>(iii) Athari za kuamini Qadar katika maisha ya kila siku. | Kufafanua dhana ya kuamaini Qadar ya Allaah (S.W) kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Matini mbalimbali kuhusu Qadar ya Allaah (S.W). | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kuisoma Qur'an kwa mazingatio ya hukumu na ujumbe. | (a) Kuchambua dhana ya usomaji wa Qur'an. *(Hukumu za lam, hukumu za qalqala, hukumu za mada, hukumu za waqfu).* | **Majadiliano**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kujadiliana kisha kuwasilisha walichojifunza juu ya:<br>(i) Hukumu za lam<br>(ii) Hukumu za qalqala<br>(iii) Hukumu za mada<br>(iv) Hukumu za waqfu | Kuchambua dhana ya usomaji wa Qur'an kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Matini mbalimbali kuhusu tajwiid. | 4 |
| | | (b) Kuchambua ithibati ya Qur'an. *(Tofauti kati ya sura za Makka na sura za Madina, ufahamu wa sababu nuzuli).* | **Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kusoma matini uliyoandaa waweze kujifunza kwa kujadiliana kisha kutoa ufafanuzi juu ya<br>(i) Tofauti kati ya sura zilizoshuka Makkah na sura zilizoshuka Madinah<br>(ii) ufahamu wa sababu nuzuli<br>Kila kundi kutoa mwakilishi kuwasilisha walichojifunza mbele ya darasa.<br>**Ramani ya Ufahamu.**<br>Andaa ramani ya dhana kuhusu sifa za sura za Makkah na zile za Madina ambapo utajaza baadhi na kuacha nyingine wanafunzi wajaze. | Kuchambua ithibati ya Qur'an kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdulla Saleh Farsy<br>- TEHAMA | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuchambua sura zilizoteuliwa: Quraysh (106), Fiil (105), Humazah (104), Asr (103). *(Kusoma kwa hukumu, kuhifadhi na kutoa mafunzo).* | **Kazimradi;**<br>Waongoze wanafunzi katika vikundi wakutane kwa muda wao wa ziada nje ya darasa kusoma kwa kuhifadhi na kutoa tafsiri ya sura zifuatazo; Quraysh (106), Al – fyl (105), Humazah (104), 'Asr (103) wabaini mafunzo katika kila sura, kisha kuwasilisha kazi zao baada ya muda uliowapa kukamilika.<br>**Majadiliano;**<br>Jadiliana na wanafunzi namna ya kutekeleza ujumbe wa sura walizojifunza. | Sura zilizoteuliwa zimechambuliwa. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Bango kitita<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdulla Saleh Farsy | 4 |
| | 1.3 Kuishi kwa kuzingatia Sunnah ya Mtume Muhammad S.A.W) | (a) Kuchambua sayansi ya Hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W). *(Aina, tanzu na uhakiki wa Hadithi).* | **Maswali na majibu na Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kusoma matini iliyoandaliwa waweze kujifunza na kufafanua<br>(i) Aina na tanzu za Hadithi.<br>(ii) Vigezo vya uhakiki wa Hadithi | Kuchambua sayansi ya Hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W). kumefanyika. | - Kitabu cha kiada<br>- kidato cha 3<br>- Matini mbalimbali kuhusu sayansi ya Hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W) | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Ramani ya Ufahamu.**<br>Andaa ramani ya ufahamu kuhusu aina na tanzu za Hadithi ambapo utajaza baadhi ya tanzu /aina na utaacha nyingine wanafunzi wajaze. | | | |
| | | (b) Kuchambua Hadithi zilizoteuliwa kuhusu kujiepusha na ria na kujiona, kujiepusha na unafiki, kuwa mwenye huruma, kuwa na haya, kudhibiti hasira, kuwa mwenye subira na uvumilivu, kuwa mkarimu, kuepuka uchoyo na ubakhili, kuwa mwenye kutosheka, kuepuka husda. *(Kusoma kwa kuhifadhi* | **Kazimradi;**<br>Waongoze wanafunzi katika vikundi wakutane kwa muda wao nje ya darasa kusoma kwa kuhifadhi, kuandika na kutoa tafsiri ya Hadithi zilizoteuliwa kuhusu kujiepusha na ria na kujiona, kujiepusha na unafiki, kuwa mwenye huruma, kuwa na haya, kudhibiti hasira, kuwa mwenye subira na uvumilivu, kuwa mkarimu, kuepuka uchoyo na ubakhili, kuwa mwenye kutosheka, kuepuka husuda.<br><br>**Matembezi ya galari;**<br>Ongoza wanafunzi kuorodhesha mafunzo yatokanayo na Hadithi husika na kubandika kwenye | Kuchambua Hadithi zilizoteuliwa kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Bango kitita<br>- Matini mbalimbali kuhusu Hadithi zilizoteuliwa.<br>- TEHAMA<br>- tafsiri ya Riyadhus Salihin. | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *kuandika, kutafsiri na kung'amua mafunzo).* | kuta za darasa, kufanya matembezi na kuuliza maswali katika vikundi mbalimbali.<br>**Fikiri - andika - jozisha - shirikisha;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kutafakari na kuandika mapendekezo namna ya kutekeleza mafunzo ya Hadithi husika kisha ufanye majumuisho. | | | |
| 2.0 Kumtumikia Allaah (S.W) katika kila kipengele cha maisha. | 2.1 Kutekeleza nguzo za Uislamu kwa kuzingatia lengo la kila nguzo. | (a) Kuchambua nguzo ya Hija *(maana, aina, umuhimu, masharti, nguzo na sunnah)* | **Bunguabongo:**<br>Waongoze wanafunzi kupitia bunguabongo kueleza maana ya hija<br>**Fikiri – jozisha – shirikisha:**<br>Waongoze wanafunzi kupitia fikiri – jozisha – shirikisha kueleza maana na aina za Hija na umuhimu wake, Maana ya Umra.<br>**Igizodhima:**<br>Waongoze wanafunzi wafanye igizo la ibada ya Hija kwa kuzingatia masharti, nguzo na Sunnah zake. | Nguzo ya Hija imechambuliwa. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3.<br>- Vitu halisi, chati/ jedwali, Qur'an tukufu | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kutathmini malengo ya nguzo za Uislamu *(namna lengo la kila nguzo linavyofikiwa, sababu za baadhi ya Waislamu kutofikia malengo ya nguzo za Uislamu)* | **Fikiri – jozisha – shirikisha:**<br>Ongoza wanafunzi kupitia fikiri – jozisha – shirikisha Kusoma matini na maswali uliyoandaa kwa kujadiliana waweze kuchambua<br>(i) Jinsi utekelezaji wa kila nguzo ya Uislamu unavyomuwezesha mja kufikia lengo<br>(ii) Kwanini baadhi ya waislamu hawafikii malengo ya nguzo za Uislamu.<br>Kila kundi kutoa mwakilishi kuwasilisha walichojifunza mbele ya wenzao darasani. | Kutathmini malengo ya nguzo za Uislamu kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Bango kitita<br>- Matini mbalimbali kuhusu Nguzo za Uislamu.<br>- TEHAMA | 2 |
| | | (c) Kuchanganua faida za utekelezaji wa nguzo za Uislamu. | **Fikiri – jozisha – shirikisha:**<br>Ongoza wanafunzi kupitia fikiri – jozisha – shirikisha kusoma matini na maswali uliyoandaa kwa kujadiliana waweze kuchanganua:<br>(i) Faida za kijamii za kila nguzo ya Uislamu<br>(ii) Faida za jumla za nguzo za Uislamu. | Kuchanganua faida za nguzo za Uislamu kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Bango kitita | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kila kundi kutoa mwakilishi kuwasilisha walichojifunza mbele ya wenzao darasani. | | | |
| | 2.2 Kuchunga mipaka ya Allaah (S.W) katika kuendesha maisha ya binafsi na jamii | (a) Kufafanua talaka na eda katika Uislamu. *(maana, hekima ya talaka, Sulhu kati ya mume na mke, aina za talaka, Taratibu za talaka, aina za eda,).* | **Changanyakete;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi kusoma matini kuhusu<br>(i) Maana na hekima ya talaka<br>(ii) Sulhu ya hitilafu zilizojitokeza baina ya mume na mke<br>(iii) Aina za talaka,<br>(iv) Taratibu za kutaliki<br>(v) Aina za eda<br>Elekeza kila kikundi kutoa mwakilishi mmoja kwenda kikundi kingine kufundisha walichojifunza katika kundi lao.<br>**Majadiliano na Kuwasilisha;**<br>Wanafunzi wakiwa katika vikundi vidogo vidogo waongoze kujadili sababu za kukithiri kwa talaka na madhara ya kifamilia na kijamii. | Kufafanua talaka na eda katika Uislamu kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Matini mbalimbali kuhusu talaka na eda katika Uislamu.<br>- Bango kitita | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuchambua malezi ya watoto baada ya ndoa kuvunjika *(mwenye haki na wajibu wa kulea, ukomo wa kulelewa watoto na haki zao)* | **Fikiri – jozisha – shirikisha:**<br>Ongoza wanafunzi kupitia fikiri – jozisha – shirikisha kusoma matini na maswali uliyoandaa kwa kujadiliana waweze kuchanganua:<br>(i) Mwenye haki na wajibu wa kulea baada ya kuvunjika ndoa.<br>(ii) Ukomo wa kulelewa watoto<br>(iii) Haki za watoto<br>Kila kundi kutoa mwakilishi kuwasilisha walichojifunza mbele ya wenzao darasani. | Kuchambua malezi ya watoto baada ya ndoa kuvunjika kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Matini mbalimbali kuhusu malezi ya watoto baada ya ndoa kuvunjika.<br>- Bango kitita | 2 |
| | | (c) Kuchambua dhana ya wasia na mirathi katika Uislamu *(maana, taratibu, masharti ya wasia na mirathi, kanuni za kugawa mirathi na kukokotoa mafungu ya mirathi kwa kufuata sharia ya Kiislamu)* | **Kumualika Mgeni;**<br>Mwalike mgeni aliye na ujuzi wa kutosha juu ya Mirathi katika Uislamu.<br>**Mwalikwa!**<br>Jadiliana na wanafunzi katika vikundi kuhusu<br>(i) Maana na taratibu za wasia. Maana ya mirathi<br>(ii) Masharti na kanuni za kugawa mirathi.<br>(iii) kukokotoa mafungu ya mirathi kwa sharia ya Kiislamu. | Kuchambua dhana ya wasia na mirathi katika Uislamu kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Matini mbalimbali kuhusu mirathi ya Kiislamu.<br>- Bango kitita | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 Kulingania na kusimamisha haki na uadilifu katika jamii. | 3.1Kutumia Qur'an na Sunnah kulingania uislamu katika jamii. | (a) Kuchambua mipango katika Da`awah *(Maana, umuhimu, hatua, vigezo, mipango ya kistratejia).* | **Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikudi kusoma matini kwa mazingatio iliyoandaliwa waweze kujifunza kwa kujadiliana juu ya<br>(i) maana na umuhimu,<br>(ii) Hatua na vigezo.<br>(iii) mipango ya kistratejia | Kuchambua mipango katika Da`awah kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Bango kitita<br>- Matini mbalimbali kuhusu mipango katika ulinganiaji. | 2 |
| | | (b) Kuchambua dhana ya uongozi bora katika kulingania uislamu *(Maana, umuhimu, aina na sifa za kiongozi wa Kiislamu).* | **Fikiri – jozisha – shirikisha:**<br>Ongoza wanafunzi kupitia fikiri – jozisha – shirikisha kusoma matini na maswali uliyoandaa kwa kujadiliana waweze kuchanganua:<br>(i) Maana ya uongozi<br>(ii) Umuhimu wa uongozi<br>(iii) Aina za uongozi<br>(iv) Sifa za kiongozi wa Kiislamu. | Kuchambua dhana ya uongozi katika kulingania kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Bango kitita<br>- Matini mbalimbali kuhusu uongozi bora katika ulinganiaji | 2 |
| | | (c) Kuchambua mafunzo na mazoezi ya kuwaandaa walinganiaji | **Fikiri -andika - jozisha -shirikisha:**<br>Ongoza wanafunzi kufikiri, kuandika, kujozisha na | Kuchambua mafunzo na mazoezi ya kuwaandaa walinganiaji kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Bango kitita<br>- Matini mbalimbali kuhusu maandalizi ya ulinganiaji. | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *(Kutoa elimu, kuilea nafsi, kujihusisha na masuala ya kijamii, kuandaa na kutoa ujumbe).* | kushirikishana katika vikundi kuchambua;<br>(i) darsa duara na kazi zake<br>(ii) Namna ya kuilea nafsi na kujihusisha na masuala ya kijamii<br>(iii) Namna ya kuandaa na kutoa ujumbe. Kisha fanya majumuisho. | | | |
| | | (d) Kuchambua hali ya Uislamu hivi sasa.<br>*(Mtawanyo wa Waislamu na wasiokuwa waislamu, mafanikio-kielimu, kiuchumi, kisiasa na kijamii, vikwazo na utatuzi wake).* | **Majadiliano;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogovidogo kuchambua<br>(i) idadi ya waislamu duniani<br>(ii) mafanikio yaliyofikiwa na uislamu duniani<br>(iii) vikwazo vinavyokwamisha harakati za kiislamu na namna ya kuvitatua.<br>kisha elekeza kila kikundi kutoa mwakilishi mmoja kwenda kikundi kingine kufundisha walichojifunza katika kundi lao kisha ufanye majumuisho. | Kuchambua hali ya Uislamu hivi sasa kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Matini mbalimbali yanayohusu hali ya uislamu duniani. | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kutumia historia ya Uislamu kujenga mwenendo mwema wa jamii. | (a) Kuchambua uanzishwaji na uendeshaji wa dola ya Kiislamu Madina.<br>*(Hali ya Madina kabla ya kuhamia Mtume Muhammad (S.A.W) kiuchumi na kisiasa, hatua alizochukua Mtume Muhammad (S.A.W) katika uanzishaji dola, mifumo ya kiuchumi, kisiasa, usalama na diplomasia).* | **Majadiliano, Maswali na Majibu;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kusoma matini uliyoandaa kwa kujadiliana kwa kuongozwa na maswali uliyoandaa waweze kufafanua kwa kina<br>(i) Hatua alizochukua Mtume Muhammad (S.A.W) kuanzisha Dola ya Kiislamu Madinah na mafunzo yatokanayo<br>(ii) Mfumo wa siasa na uchumi, diplomasia, ulinzi na usalama wa dola ya Kiislamu Madinah na Mafunzo yatokanayo.<br>Kila kundi kutoa mwakilishi kuwasilisha walichojifunza mbele ya wenzao darasani. | Kuchambua uanzishwaji na uendeshaji wa dola ya Kiislamu Madina kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Bango kitita<br>- Matini mbalimbali kuhusu uanzishwaji na uendeshaji wa dola ya Kiislamu Madina.<br>- TEHAMA | 4 |
| | | (b) Kuchambua upinzani dhidi ya Dola ya Kiislamu Madina.<br>*(vita vya Badri, vita vya Uhud, vita vya* | **Majadiliano, Maswali na Majibu;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kusoma matini uliyoandaa kwa kujadiliana kwa kuongozwa na | Kuchambua upinzani dhidi ya dola ya Kiislamu Madina kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Bango kitita<br>- Matini mbalimbali kuhusu upinzani dhidi ya Dola ya Kiislamu Madina. | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *Ahzab, uadui wa Mayahudi, vita vya Hunein, hatua zilizochukuliwa na Mtume Muhammad (S.A.W) mafunzo yatokanayo).* | maswali uliyoandaa wawezi kufafanua:<br>(i) Mbinu za maadui<br>(ii) hatua zilizochukuliwa (mikataba – Madina na makabila ya kiyahudi nje ya madina, diplomasia na mapambano – Badri, Uhud, Ahzab na Hunein)<br>(iii) Mafunzo yatokanayo na mbinu za maadui na hatua zilizochukuliwa.<br>Kila kundi kutoa mwakilishi kuwasilisha walichojifunza mbele ya wenzao darasani. | | | |
| | | (c) Kubainisha ushindi wa Waislamu (Fat-hu- Makkah).<br>*(Mkataba wa Hudaybiyya, kukombolewa mji wa Makka msafara wa Tabuuk, Hija ya kuaga na Mafunzo yatokanayo).* | **Majadiliano, Maswali na Majibu;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kusoma matini uliyoandaa kwa kujadiliana kwa kuongozwa na maswali uliyoandaa wawezi kufafanua kwa kina<br>(i) Mazingira yaliyopelekea mkataba wa Hudaybiyah<br>(ii) Vifungu vya mkataba | Kubainisha ushindi wa waislamu (Fat-hu- Makkah). kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 3<br>- Bango kitita<br>- Matini mbalimbali kuhusu ushindi wa waislamu (Fat-hu- Makkah). | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | (iii) Msafara wa Tabuk<br>(iv) Hija ya kuaga ya Mtume Muhammad (S.A.W)<br>(v) Mafunzo yatokanayo na mkataba wa hudaibiya na msafara wa Tabuk.<br>Kila kundi kutoa mwakilishi kuwasilisha walichojifunza mbele ya wenzao darasani. | | | |

## Kidato cha IV

**Jedwali Na. 6:** *Maudhui ya Kidato cha IV*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumtambua, kumpenda, kumtukuza na kumsifu Allaah (S.W). | 1.1 Kutambua uwepo wa Allaah (S.W) na sifa zake. | (a) Kueleza Itikadi, udhaifu na athari za dini zilizoundwa na watu. *(Ukafiri, ushirikina-ukristo na uyahudi, na utawa-ubudha, uhindu)* | **Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kujadiliana juu ya athari ya ukafiri, ushirikina na utawa) katika jamii. | Kueleza Itikadi, udhaifu na athari ya dini zilizoundwa na watu kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Bango kitita<br>- Matini mbalimbali kuhusu athari ya dini za watu.<br>- TEHAMA | 4 |
| | | (b) Kujadili vigezo vya dini sahihi anayostahiki mwanadamu. | **Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kujadiliana juu ya vigezo vya dini anayostahiki mwanadamu. | Vigezo vya dini sahihi anayostahiki mwanadamu vimejadiliwa. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Bango kitita<br>- Matini mbalimbali kuhusu vigezo vya dini sahihi.<br>- TEHAMA. | 4 |
| | 1.2 Kuisoma Qur'an kwa mazingatio ya hukumu na ujumbe. | (a) Kufafanua Ithibati ya Qur'an. *(Hoja za kuthibitisha kuwa Qur'an ni Kitabu cha Allaah (S.W) na udhaifu wa madai ya wapinzani dhidi ya Qur'an).* | **Maswali na Majibu;** Ongoza wanafunzi kwa kuuliza maswali ili kuwawezesha kujadiliana katika vikundi vyao kutoa ushahidi wa ndani na nje ya Qur'an kuthibitisha kuwa Qur'an ni kitabu cha Allaah (S.W). | Kufafanua Ithibati ya Qur'an kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuchambua sura zilizoteuliwa:<br>Tyn (95),<br>Nashrah (94)<br>Takaathur (102)<br>Al-Bayyinah, (98)<br>Adh Dhuhaa (93)<br>Al-A'alaa (87)<br>*(Kusoma kwa kuhifadhi, kutafsiri, kutoa mafunzo yatokanayo).* | **Kazimradi;**<br>Waongoze wanafunzi katika vikundi wakutane kwa muda wao wa ziada nje ya darasa kusoma kwa kuhifadhi na kutoa tafsiri ya sura zilizoteuliwa: Tyn, Nashrah, Bayinnah, Takaathur, Dhuhaa na A'alaa.<br>Wabaini mafunzo kutoka katika kila sura kisha kuwasilisha kazi zao baada ya muda uliowapa kukamilika.<br>**Majadiliano.**<br>Jadiliana na wanafunzi namna ya kutekeleza ujumbe wa sura walizojifunza. | Kuchambua Sura zilizoteuliwa kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Tafsiri ya Qur'an Sheikh Abdullah Saleh Farsy | 8 |
| | 1.3 Kuishi kwa kuzingatia Sunnah ya Mtume Muhammad (SAW) | (a) Kuchambua kukubalika kwa Hadithi.<br>*(Hoja za kukubalika na udhaifu wa hoja za wapinzani wa Hadithi)* | **Majadiliano:**<br>Ongoza wanafunzi katika vikudi kusoma matini iliyoandaliwa kwa mazingatio waweze kujifunza kwa kujadiliana juu ya<br>(i) Hoja za kukubalika kwa Hadithi<br>(ii) Udhaifu wa hoja za wapinzani wa Hadithi | Kuchambua kukubalika kwa Hadithi kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4 | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuchambua Hadithi zilizoteuliwa kuhusu kuwa na Hekima, kuepuka tamaa na kuombaomba, kumtegemea Allaah (S.W), kuepuka kukata tamaa, kuwa na Istiqama.<br>*(Kusoma kwa kuhifadhi, kuandika, kutafsiri na kubaini mafunzo).* | **Kazimradi;**<br>Waongoze wanafunzi katika vikundi wakutane kwa muda wao nje ya darasa kusoma kwa kuhifadhi, kuandika na kutoa tafsiri ya Hadithi zilizoteuliwa kuhusu kuwa na Hekima, kuepuka tamaa na kuombaomba, kumtegemea Allaah (S.W), kuepuka kukata tamaa, kuwa na Istiqama.<br>**Matembezi ya galari;**<br>Ongoza wanafunzi kuorodhesha mafunzo yatokanayo na Hadithi husika na kubandika kwenye kuta za darasa, kufanya matembezi na kuuliza maswali katika vikundi mbalimbali.<br>**Fikiri - andika - jozisha - shirikisha;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kutafakari na kuandika mapendekezo namna ya kutekeleza mafunzo ya Hadithi husika kisha ufanye majumuisho. | Kuchambua Hadithi zilizoteuliwa kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Tafsiri ya Riyadhus Salihina. | 6 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kumtumikia Allaah (S.W) katika kila kipengele cha maisha. | 2.1 Kutekeleza nguzo za Uislamu kwa kuzingatia lengo la kila nguzo. | (a) Kuandaa na kutoa khutba za Ijumaa na Eid *(Maana, umuhimu, masharti, nguzo, sunnah na adabu).* | **Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikudi kusoma kwa mazingatio matini iliyoandaliwa ili waweze kujifunza kwa kujadiliana juu ya nguzo na taratibu za kuandaa na kutoa khutba ya Ijumaa na khutba ya Eid.<br>**Igizo dhima:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kufanya igizo la utoaji wa khutba ya ijumaa na khutba ya Eid. | Kuandaa na kutoa khutba za Ijumaa na Eid kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Matini mbalimbali kuhusu khutbah za Ijumaa na Eid. | 2 |
| | | (b) Kuandaa na kutoa khutba ya ndoa *(Maana, umuhimu, masharti, nguzo, sunnah na adabu)* | **Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikudi kusoma matini kwa mazingatio iliyoandaliwa waweze kujifunza kwa kujadiliana juu ya nguzo na taratibu za khutba ya ndoa.<br>**Igizo dhima:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kufanya igizo la utoaji wa khutba ya ndoa. | Uandaaji na utoaji wa khutbah ya ndoa umefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Matini mbalimbali kuhusu khutbah ya ndoa. | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kuchunga mipaka ya Allaah (S.W) katika kuendesha maisha ya binafsi na jamii. | (a) Kufafanua dhana ya kudhibiti uzazi katika Uislamu *(Maana, udhaifu wa hoja za wanaoendesha kampeni ya kudhibiti uzazi, mtazamo wa Uislamu juu ya kudhibiti uzazi).* | **Maswali na Majibu;** Ongoza wanafunzi katika vikundi kwa maswali waweze kujadiliana na kuchambua<br>(i) Maana ya kudhibiti uzazi<br>(ii) Hoja na udhaifu wa wanaoendesha kampeni ya kudhibiti uzazi<br>(iii) Mtazamo wa Uislamu juu ya kudhibiti uzazi. | Kufafanua dhana ya kudhibiti uzazi katika Uislamu kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4.<br>- Matini mbalimbali kuhusu mirathi<br>- Bango kitita | 2 |
| | | (b) Kuchambua hadhi na haki za mwanamke katika Uislamu *(tofauti ya hadhi na haki za mwanamke katika Uislamu na jamii za kijahili, hifadhi ya mwanamke katika Uislamu).* | **Utafiti Mdogo;** Elekeza wanafunzi wakiwa katika makundi yao wakasome matini na kuchunguza kisha kuandika taarifa kuhusu<br>(i) Tofauti ya hadhi na haki za mwanamke katika Uislamu na jamii za kijahili.<br>(ii) Hifadhi ya mwanamke katika Uislamu | Kuchambua hadhi na haki za mwanamke katika Uislamu kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4.<br>- Matini mbalimbali kuhusu familia ya Kiislamu<br>- Bango kitita | 2 |
| | | (c ) Kuchambua sharia za Kiislamu. *(Maana ya sharia, tofauti kati ya sharia* | **Majadiliano;** Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo wafafanue | Kuchambua sharia ya Kiislamu kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Matini mbalimbali kuhusu sharia za Kiislamu | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | *za Kiislamu na sheria za kikafiri, misingi ya halali na haramu katika Uislamu, makosa na adhabu katika sharia za Kiislamu).* | (i) tofauti ya chimbuko la sharia za Kiislamu na chimbuko la sheria za kikafiri<br>(ii) Kazi za sharia<br>(iii) Makosa na adhabu zake katika Uislamu. | | - Bango kitita.<br>- TEHAMA | |
| | | (d) Kufafanua siasa na uchumi katika Uislamu.<br>*(tofauti kati ya Uislamu na ukafiri juu ya mtazamo wa siasa na dola, Tofauti ya msonge wa uongozi wa Kiislamu na uongozi wa kikafiri, tofauti kati ya mfumo wa uchumi wa Kiislamu na mfumo wa uchumi wa kikafiri, uchumi halali na haramu, uharamu wa riba, misingi ya mifumo ya kifedha ya Kiislamu).* | **Changanyakete;**<br>Ongoza wanafunzi katika vikundi kusoma matini kuhusu<br>(i) tofauti kati ya Uislamu na ukafiri juu ya mtazamo wa siasa na dola.<br>(ii) tofauti ya msonge wa uongozi wa Kiislamu na uongozi wa kikafiri<br>(iii) tofauti kati ya mfumo wa uchumi wa Kiislamu na ule wa kikafiri<br>(iv) Uchumi halali na haramu katika Uislamu<br>(v) Uharamu wa riba<br>(vi) Mifumo ya kifedha ya Kiislamu: benki za Kiislamu, bima za Kiislamu n.k).<br>kisha elekeza kila kikundi kutoa mwakilishi mmoja kwenda kikundi kingine kufundisha walichojifunza katika kundi lao kisha ufanye majumuisho. | Kufafanua siasa na uchumi katika Uislamu kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4.<br>- Matini juu ya siasa na uchumi katika Uislamu.<br>- Bango kitita | 6 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 Kulingania na kusimamisha haki na uadilifu katika jamii. | 3.1 Kutumia Qur'an na Sunnah kulingania uislamu katika jamii. | (a) Kuchambua nyanja za kulingania uislamu *(Uongozi, itikadi, tarbia, wito kwa wasiokuwa Waislamu na ulinzi).* | **Majadiliano na kuwasilisha;** Ongoza wanafunzi watumie matini katika vikundi vidogo vidogo wachambue nyanja za kulingania ambazo ni Uongozi, itikadi, tarbia, wito kwa wasiokuwa Waislamu na ulinzi. Baada ya kila kikundi kuwasilisha mbele ya wenzao kujadiliana wote darasani ufanye majumuisho. | Kuchambua nyanja za kulingania kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Matini juu nyanja za, kulingania jamii.<br>- Bango kitita | 2 |
| | | (b) Kufafanua nyenzo za kulingania *(Qur'an na Hadithi, vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, vitabu, nk).* | **Majadiliano na kuwasilisha;** Ongoza wanafunzi watumie matini katika vikundi vidogo vidogo wachambue nyenzo za kulingania zinavyoweza kutumika kufikia lengo la kulingania. | Kufafanua nyenzo za kulingania kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Matini mbalimbali yanayohusu nyenzo za kulingania<br>- Kitabu cha Riyadhu Salihin.Qur'an Tukufu. | 2 |
| | | (c) Kuchambua njia na mbinu za kulingania *(semina, itkaf, vituo vya elimu, vituo vya, dhifa, mikutano).* | **Majadiliano na kuwasilisha;** Ongoza wanafunzi watumie matini katika vikundi vidogo vidogo wachambue mbinu za kulingania zinavyoweza kufikiwa lengo la kulingania. | Kuchambua njia na mbinu za kulingania kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Matini mbalimbali yanayohusu njia na mbinu za kulingania | 2 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kueleza mbinu zinazotumika kupiga vita Uislamu na namna muislamu anavyotakiwa kuishi na wasiokuwa Waislamu *(kiuchumi, kiutamaduni, kijamii, kisiasa na kielimu* | **Majadiliano na kuwasilisha;** Ongoza wanafunzi watumie matini katika vikundi vidogo vidogo wachanganue<br>(i) Mbinu zinazotumika kupiga vita Uislamu.<br>(ii) Namna ya muislamu anavyotakiwa kuishi na wasiokuwa Waislamu.<br>*(Kiuchumi, kijamii, kisiasa na kielimu.* | Kueleza mbinu zinazotumika kupiga vita Uislamu na namna muislamu anavyotakiwa kuishi na wasiokuwa Waislamu kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Matini mbalimbali yanayohusu mbinu zinazotumika kupiga vita Uislamu na namna muislamu anavyotakiwa kuishi na wasiokuwa Waislamu. | 2 |
| | 3.2 Kutumia historia ya Uislamu kujenga mwenendo mwema wa jamii | (a) Kutathmini uendeshaji wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa. *(Taratibu zilizotumika kuwapata makhalifa, sababu za kupanuka Dola ya Kiislamu, sababu za Riddah, mfumo wa uongozi, uchumi, ulinzi na mahusiano ya kimataifa, sababu za kuporomoka dola ya Kiislamu na mafunzo yatokanayo katika kuimarisha umma).* | **Majadiliano na kuwasilisha;** Ongoza wanafunzi watumie matini katika vikundi vidogovidogo wachanganue<br>(i) Taratibu zilizotumika kuwapata makhalifa wanne waongofu<br>(ii) Sababu za kupanuka dola ya Kiislamu wakati wa makhalifa<br>(iii) sababu zilipolekea Riddah<br>(iv) Mfumo wa uongozi, uchumi, ulinzi na mahusiano ya kimataifa wakati wa makhalifa | Kutathmini uendeshaji wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Matini mbalimbali kuhusu Historia ya Uislamu wakati wa Makhalifa<br>- TEHAMA | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | (v) Sababu zilizopelekea kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu na mafunzo yatokanayo katika kuimarisha umma. | | | |
| | | (b) Kutathmini harakati za kuendeleza Uislamu baada ya makhalifa *(Banu Umayya, Abasid, Uthmaniyya, mughals:- mbinu, mafanikio, changamoto, mafunzo).* | **Kazimradi;** Andaa maswali ya kuwangoza wanafunzi katika vikundi vidogo vidogo kuchunguza na kuandika taarifa juu ya harakati za kuendeleza Uislamu baada ya makhalifa na mafunzo yatokanayo.<br>**Changanyakete;** Elekeza kila kikundi kutoa mwakilishi mmoja kwenda kikundi kingine kufundisha walichojifunza katika kundi lao kisha wajadiliane kisha ufanye majumuisho. | Tathmini ya harakati za kuendeleza Uislamu baada ya makhalifa imefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Matini mbalimbali kuhusu historia ya harakati ya kuendeleza Uislamu baada ya Makhalifa | 6 |
| | | (c) Kufafanua kuenea kwa Uislamu Tanzania *(Njia zilizotumika, dola ya Kilwa, dola ya Zanzibar, Uislamu wakati na baada ya ukoloni hadi hivi leo).* | **Majadiliano na kuwasilisha;** Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogovidogo kwa maswali, kusoma matini ili kuwawezesha kufafanua<br>(i) Njia zilizotumika kufikisha Uislamu Tanzania | Kufafanua kuenea kwa Uislamu Tanzania kumefanyika. | - Kitabu cha kiada kidato cha 4<br>- Matini za Historia ya Uislamu Tanzania.<br>- TEHAMA | 4 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | (ii) dola ya Kilwa<br>(iii) dola ya Zanzibar<br>(iv) Uislamu wakati ukoloni<br>(v) Uislamu baada ya ukoloni<br>(vi) Mafunzo yatokanayo na jitihada za kuendeleza Uislamu Tanzania.<br>Baada ya kila kikundi kuwasilisha mbele ya wenzao kujadiliana wote darasani kisha ufanye majumuisho. | | |

## Bibliografia


*Farsy. A .S (1987). Tafsiri ya Kiswahili ya Qur'an Tukufu. The Islamic Foundation (Nairobi, Kenya). Muhammad Abdallah Swaleh, (2018)*

*Islamic Education Panel (2012). Muhutasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Kidato cha I-IV. Islamic Education Panel (Dar es Salaam).*

*Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), (2019) Kamusi ya Kiswahili sanifu, Chuo kikuu cha Dar es Salaam (Dar es Salaam, Tanzania)*

*Tafsiri ya Kiswahili ya Riyadhus Salihiin, chapa ya pili.(2018) Ibn Hazm Media Center (Dar es Salaam).*